



MUHTASARI

- Katika kipindi cha Machi 21-31 2024, hali ya mvua inatarajiwa katika maeneo mengi nchini ambayo itasaidia ukuaji na maendeleo ya mazao
- Wakulima katika maeneo yanayopata mvua za Masika wanashauriwa kuendelea kupanda mazao huku wakipata ushauri kutoka kwa maafisa kilimo katika maeneo yao
- Wakulima na wafugaji wanashauriwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao, mashamba, mifugo na malisho ili kuweza kukabiliana na athari mbalimbali zinazoweza kujitokeza.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2024


Migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene iliimarika kidogo wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipungua nguvu kidogo. Hali hii ilisababisha ukanda mvua (ITCZ) kusogea kidogo kuelekea kaskazini na kuwepo katika baadhi ya maeneo nchini.

Joto la bahari la juu ya wastani liliendelea kusambaa katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi hususan katika eneo la Rasi ya Msumbiji, hali hii ilichangia kusababisha kutengenezwa kwa migandamizo midogo ya hewa. Migandamizo hiyo midogo ya hewa iliimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya pwani ya kusini, nyanda za juu kusini magharibi na kusini mwa nchi na kudhohofisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo yaliyopo kaskazini hasa nyanda za juu kaskazini na maeneo jirani.

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea kuwepo kwa vipindi vya mvua zilizoambatana na ngurumo za radi katika maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria, magharibi, kusini, nyanda za juu kusini magharibi na katika maeneo ya ukanda wa Pwani.

TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2024

Katika kipindi hiki, maeneo mengi nchini yalipata mvua kiasi cha milimita (mm) 10 hadi mm 100 za mvua isipokuwa katika maeneo mengi ya mikoa wa Arusha, Mara, Ruvuma, Geita, Kagera, Tabora, Singida na Dodoma mbayo yalipata mvua chini ya milimita 10 kama inavyo onekana kwenye Kielelezo.



Kielelezo 1: Kiasi cha mvua kwa siku 10 kwa kipindi cha Machi 11-20, 2024

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MACHI 11-20, 2024

Katika dikadi hii, mvua zilizonyesha katika baadhi ya maeneo nchini zilisaaidia ukuaji na maendeleo ya mazao.

Maeneo yanayopata mvua za Masika, wakulima waliendelea na shughuli za kupanda mazao hususan mahindi na kufanya maandalizi ya mashamba ya kupanda alizeti.

Katika maeneo yanayopata mvua za Msimu hususan katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Dodoma Mbeya, Iringa, Ruvuma, na Rukwa, mahindi yapo katika hatua ya kubeba na kukomaa isipokuwa katika mikoa wa Njombe ambako mahindi yapo katika hatua kati ya kubumba na kutoa mbelewele.

Zao la mpunga lipo katika hatua ya kukua hususan kwa maeneo ya mikoa ya Rukwa, Tabora, Mbeya, Shinyanga, na Morogoro na wakulima wameendelea na palizi.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyama ulikuwa wa kutosha katika maeneo mengi nchini.

**HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA
MACHI 11-20, 2024**

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mabonde kimeendelea kuongezeka kutokana na mvua zinazoendelea.

**MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA
KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2024**

Katika dekadhi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuimarika kidogo wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kupungua nguvu kidogo. Hali hii inatarajiwa kusababisha ukanda mvua (ITCZ) kuendelea kubakia katika baadhi ya maeneo nchini.

Joto la bahari katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la juu kidogo ya wastani hususan katika eneo la kaskazini mwa Madagascar, hali hii inatarajiwa kusababisha uwepo wa migandamizo midogo ya hewa na hivyo kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani hususan katika kipindi cha nusu ya kwanza ya dekadhi.

**HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA
KIPINDI CHA MACHI 21-31,2024**

Maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida), na mikoa ya magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara, na Kilimanjaro), kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro) na pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) yanatarajiwa kuwa na mvua zitazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani, na Dar es Salaam vikiwemo visiwa vya Unguja na Pemba), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) yaatarajiwa kuwa na mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

vua zinazotarajiwa katika maeneo mengi nchini zitasaidia kuongeza unyevunyevu katika udongo ambao utasaidia katika ukuaji na maendeleo ya mazao. Hata hivyo, mvua hizo zikiwa nyingi zinaweza kuathiri ukuaji wa mazao hayo.

Wakulima katika maeneo yanayopata mvua za Masika wanashauriwa kuendelea kupanda mazao huku wikipata ushauri kutoka kwa maafisa kilimo katika maeneo yao.

**HALI YA HEWA KILIMO:
MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI
CHA MACHI 21-31, 2024**

Katika maeneo yanayopata mvua za Msimu, wakulima wanashauriwa kufuatilia kwa ukaribu hali ya mazao ili kuweza kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na hali ya hewa inayotarajiwa, milipuko ya wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea pale vitakapojitokeza.

Wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, hususan kwenye bahari ya Hindi na Maziwa Makuu ili kufanya maamuzi na mipango sahihi kwa ajili ya shughuli za uvuvi. Wafugaji wanashauriwa kupanda majani ya kutosha na kuchimba mabwawa ya kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadai

**HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA
KIPINDI CHA MACHI 21-31,2024**

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kuongezeka kutokana na mvua zinazoendelea.

Jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa matumizi ya baadaye.